# Bajaji 5,000 zinatumia gesi asili nchini-TPDC

Na Anne Robi Mtwara

SHIRIKA la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) limesema bajaji zaidi ya 5,000 nchini kwa sasa zinatumia nishati safi ya gesi asilia (CNG).

Ofisa Maendeleo ya Jamii Mwandamizi wa TPDC, Ally Mluge alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari katika Maonesho ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi maarufu Nanenane Kanda ya Kusini mkoani Lindi.

"Kwa sasa zaidi ya bajaji 5,000 na magari 5,000 nchini yanatumia nishati safi ya gesi asilia," alisema.

Idadi ya vituo vya kujazia gesi asilia kwenye magari na bajaji vimefika vinane kikiwemo kituo kikubwa cha jijini Dar es Salaam chenye uwezo wa kujaza gesi asilia kwenye magari 1,200 kwa siku.

"Ujenzi wa kituo hicho umekamilika na kinatoa huduma ya kujaza gesi kwenye magari, bajaji ambapo kimesaidia hata kupunguza msongamano wa vyombo vya moto vinatumia nishati hiyo kwenye vituo vingine," alisema.

Akizungumzia mkakati wa Matumizi ya Nishati Safi ya kupikia, Mluge alisema nyumba zaidi ya 1,522 na taasisi 13 Dar es Salaam, Lindi na Mtwara zimeunganishwa na matumizi ya nishati hiyo.

Mkakati huo pia umeunganisha viwanda 57 huku mchakato ukiendelea kuunganisha viwanda vingine zaidi.

Mluge alisema mkakati huo wenye lengo la kuunganisha asilimia 80 ya watanzania kwenye matumizi ya nishati safi ya gesi asilia ifikapo mwaka 2034 unaendelea katika mkoa wa Lindi na Mtwara.

Upande wa Lindi, Mluge alisema nyumba 470 zinatarajia kuunganishwa kupitia utekelezaji wa mradi wa pili ambao unatakelezwa katika eneo la Mnazi mmoja. mradi wa kwanza uliunganisha nyumba 209.

Mluge alisema mradi huo utaunganisha nishati kwa nyumba 570 eneo la Kisemvule Wilaya ya Mkuranga, mkoani Pwani.

Kwa upande wa Mtwara nyumba 420 zimekwisha kuunganishwa na nishati hiyo.

Ili kuhakikisha kuwa mkakati wa nishati safi ya kupikia unatakelezwa, Mluge alisema TPDC wanashirikiana na Wakala wa Nishati Vijijini ili kutekeleza malengo ya mkakati wa matumizi ya nishati safi ya kupikia ifikapo 2034.

"Mpango wa TPDC ni kuendelea kusambaza nishati hiyo maeneo mengi," alisema na kuongeza kuwa kwa sasa TPDC wanashirikiana na Wakala wa vijijini kutekeleza Mikakati (REA).



Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anamringi Macha akifanya usafi mjini Bariadi juzi. (Picha na Erick Milton).

Scanned with CamScanner